## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI OKTOBA, 2025 NA MWELEKEO KWA MWEZI NOVEMBA, 2025.

**Dondoo za tathmini ya Oktoba, 2025 na mwelekeo wa Novemba, 2025:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Oktoba, 2025 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Novemba, 2025 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2025 vipindi vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ikiashiria kuanza kwa mvua za Vuli, 2025 katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria. Aidha, vipindi vichache vya mvua kubwa vilijitokeza.

ii. Katika kipindi cha mwezi Novemba 2025, mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza katika baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Aidha, mvua za Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo ya ukanda wa pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki.


iii. Hali ya joto inatarajiwa kuendelea katika maeneo yanayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2025.

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2025 vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo viliripotiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, ikiashiria kuanza kwa mvua za Vuli, 2025 kama ilivyotabiriwa. Aidha, vipindi vya mvua zenye mtawanyiko na mwendelezo usioridhisha vilijitokeza katika maeneo ya mwambao wa pwani na magharibi mwa nchi. Ongezeko kidogo la mvua lilijitokeza katika maeneo ya mwambao wa pwani kuelekea mwishoni mwa mwezi, kutokana na mabaki ya mawingu mazito ya mvua ya kimbunga “*Chenge*”. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 193.2 kilipimwa katika

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

kituo cha hali ya hewa Matangatuani (Kisiwani Pemba) mnamo tarehe 29 Oktoba, 2025. Kwa upande mwingine, hali ya joto iliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 35.5 °C kiliripotiwa katika kituo cha hali ya hewa Mpanda (mkoa wa Katavi) mnamo tarehe 16 Oktoba, 2025. Vituo vilivyopima mvua milimita 50 au zaidi ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba 1 hapo chini;




Kielelezo 1: Vituo vilivyopima viwango vya mvua milimita 50 au zaidi katika mwezi Oktoba, 2025

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI NOVEMBA, 2025

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2025 joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la chini ya wastani, ikiashiria uwepo wa

hali ya La Niña hafifu. Aidha, joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani, na eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kupunguza uwepo wa upepo wenye unyevu unaovuma kuelekea ukanda wa pwani pamoja na mikoa ya jirani. Hali ya joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani inatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango wa kusababisha upepo wenye unyevu kutoka misitu ya Congo kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI NOVEMBA, 2025

Katika kipindi cha mwezi Novemba 2025, mvua za Msimu, 2025/2025 zinatarajiwa kuanza katika baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka mvua za msimu zinatarajiwa kuanza katika maeneo ya ukanda wa pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki. Hata hivyo, mtawanyiko wa mvua unatarajiwa kuwa hafifu na kusuasua katika baadhi ya maeneo. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache nchini. Kwa upande mwingine, hali ya joto ya inatarajiwa kuendelea kujitokeza hususan katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili na ya tatu ya mwezi.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili na ya tatu.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Kwa ujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili na ya tatu.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua katika maeneo machache linatarajiwa wiki ya pili ya mwezi.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI DISEMBA, 2025

Katika kipindi cha mwezi Disemba, 2025 vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya nyakati. Hali ya joto inatarajiwa kuendelea katika maeneo yanayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua.

## 2.4 USHAURI

Mvua za msimu zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza. Hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko mara kwa mara au jirani na maeneo hayo wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na mvua kubwa ikiwemo hatari ya mafuriko.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Novemba, 2025 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz